**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS-MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA**

**WAKALA YA SERIKALI MTANDAO (eGA)**



# Taarifa ya Kikao Kazi cha Pili cha Serikali Mtandao 2019

**UDOM – CIVE Dodoma.**

**30 Januari - 2 Februari, 2019**

# YALIYOMO

**YALIYOMO** ........ i

**1.0 MUHTASARI** ........ 1

**UTANGULIZI** ........ 3

**2.1 Lengo la Kikao Kazi** ........ 3

**2.2 Kauli mbiu** ........ 3

**2.3 Ukumbi na Tarehe ya Kikao Kazi** ........ 3

**2.4 Washiriki** ........ 3

**2.4.1 Kundi la Kwanza 30 - 31/01 – 2019** ........ 3

**2.4.2 Kundi la Pili 01 Februari 2019** ........ 4

**2.4.3 Kundi la Tatu 02 Februari 2019** ........ 4

**2.5 Ufadhili wa Kikao Kazi** ........ 4

**2.6 Ada ya Ushiriki** ........ 4

**2.7 Maonesho** ........ 4

**2.8 Kamati za Maandalizi ya Kikao Kazi** ........ 4

**3.0 UFUNGUZI NA UFUNGAJI** ........ 6

**3.1 Ufunguzi wa Kikao Kazi Kundi la Kwanza 30/01/2019** ........ 6

**3.2 Ufunguzi wa Kikao Kazi kwa Kundi la Pili: 01/02/2019** ........ 7

**3.3 Ufungaji wa Kikao Kazi** ........ 8

**4.0 UWASILISHAJI WA MADA** ........ 9

**4.1 Kundi la Kwanza 30/01 - 02 /02/2019.** ........ 9

**4.1.1 Mada I: Utekelezaji wa Serikali Mtandao Nchini** ........ 9

**4.1.2 Mada II: Taarifa ya Utekelezaji wa Serikali Mtandao – Kila Wizara** ........ 10

Jedwali I: Wizara zilizowasilisha Taarifa ........ 10

Jedwali II: Wizara ambazo hazikuwasilisha Taarifa ........ 11

**4.2 Kundi la Pili 01/02/2019** ........ 12

**4.2.1 Maoni na Hoja (Key Issues) zilizojitokeza katika Utekelezaji wa Serikali Mtandao – Kundi la Kwanza** ........ 13

**4.3 Majadiliano katika Vikundi (Breakout Session)** ........ 13

**4.5 Kundi laTatu: Siku Maalumu ya Utafiti na Ubunifu wa Serikali Mtandao** ........ 14

Jedwali Na.3 Taasisi zilizowasilisha Tafiti /Bunifu ........ 15

**5.0 MAMBO MUHIMU YA KUJIFUNZA** ........ 18

**HITIMISHO** ........ 19

**VIAMBATISH0** ..... **20**
**Kiambatisho I: Ratiba ya Kikao Kazi cha Pili cha Serikali Mtandao 2019** ..... **20**
**Kiambatishi II: Hotuba** ..... **26**

# 1.0 MUHTASARI

Serikali imefanya jitihada mbalimbali katika utekelezaji wa serikali mtandao nchini ikiwemo kuandaa, kuendesha, kusimamia miundombinu na mifumo ya TEHAMA na utekelezaji wa miongozo na viwango vya serikali mtandao. Lengo la jitihada hizo ni kuhakikisha kuwa matumizi ya TEHAMA Serikalini yanakuwa na tija na kuongeza ufanisi, uwazi, uwajibikaji na ubora katika utoaji wa huduma kwa umma kwa gharama nafuu.

Pamoja na jitihada hizo, changamoto mbalimbali zimekuwa zikijitokeza katika utekelezaji wa Serikali Mtandao. Hivyo, Wakala ya Serikali Mtandao (eGA) iliandaa Kikao Kazi cha pili cha Serikali Mtandao kilichofanyika **Januari 30 hadi Februari 2, 2019** katika Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) katika ukumbi wa Chuo cha Sayansi ya Kompyuta, Habari na Mawasiliano ili wadau wa serikali mtandao waweze kubadilishana uzoefu, kujadili njia mbalimbali za kutatua changamoto na kuwa na uelewa wa pamoja kuhusu serikali mtandao.

Kikao hicho kilihudhuriwa na washiriki 786 kutoka taasisi za umma waliogawanyika katika makundi matatu. Kundi la kwanza lilifanya kikao tarehe 30 - 31 Januari, 2019 ambalo lilihusisha Maofisa TEHAMA na Maofisa wanaotumia mifumo ya TEHAMA. Kundi la pili lilifanya kikao cha tarehe 01 Februari 2019 na lilihusisha Makatibu Wakuu, Wakuu wa Taasisi na Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kundi la tatu lilihuhusisha washiriki wa makundi yote (Kundi la kwanza na la pili) pamoja na Wabunifu na Watafiti kutoka Vyuo Vikuu na Vyuo vinavyotoa mafunzo ya Teknolojia. Kundi hili la tatu lilihudhuria Kikao cha siku maalumu ya Utafiti na Ubunifu katika eneo la utekelezaji wa Serikali Mtandao tarehe 2 Februari 2019.

Wakati wa Kikao kazi hiki, taarifa inayoonesha jitihada mbalimbali za Serikali Mtandao zilizofanyika, zinazoendelea na zilizopangwa kufanyika ndani ya Serikali, changamoto na fursa zilizopo zakuzitatua iliwasilishwa. Aidha Taarifa za Utekelezaji wa Serikali Mtandao kutoka katika Wizara 16 kati ya Wizara 22 ziliwasilishwa wakati wa kikao cha kundi la kwanza. Wadau walijadiliana na kutoa mapendekezo ya jinsi ya kutatua changamoto zinazojitokeza katika utekelezaji wa jitihada za Serikali mtandao nchini. Kikao cha kundi la pili cha tarehe 1/2/2019 kilichohusisha Maafisa Masuuli kutoka taasisi za umma walijadili mapendekezo hayo na kutoa ushauri wa jinsi ya kutatekeleza.

Mapendekezo muhimu yaliyojitokeza katika utekelezaji wa Serikali Mtandao ni pamoja na Kuendelea kusimamia Miongozo na Viwango vya Serikali Mtandao; Kutoa kipaumbele katika mifumo ya TEHAMA inayosanifiwa na kutengenezwa na wataalamu wa ndani; Kuimarisha usimamizi wa usalama wa mifumo ya TEHAMA; Kuongeza jitihada za Serikali Mtandao kwa kutengeneza mifumo shirikishi ya TEHAMA ya kimkakati hususan kutoka Serikali kwenda kwa wananchi (G2C) na wafanyabiashara (G2B); Kuishauri Serikali kusaidia kutatua changamoto za Fedha na Rasilimali watu; Kushirikisha vyuo vikuu katika kufanya tafiti za miradi ya TEHAMA katika Taasisi za umma

Aidha, Washiriki waligawanyika katika makundi na kujadiliana changamoto hizo kwa kina na kuainisha mbinu na fursa ikiwemo kuandaa mpango kazi utakao ongeza ufanisi na tija katika utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao.

Aidha, Katika Kikao cha kundi la tatu ambacho kilikuwa maalum kwa ajili ya Utafiti na Ubunifu wa Serikali Mtandao, ambapo Vyuo Vikuu, Vyuo vinavyotoa mafunzo ya Teknolojia na Taasisi za Utafiti nchini vilialikwa kuwasilisha bunifu na tafiti katika serikali mtandao. Jumla ya Tafiti/Bunifu 24 ziliwasilishwa. Tafiti/Bunifu 10 zilichaguliwa kushiriki maonesho wakati wa kikao kazi hicho. Aidha Tafiti/Bunifu nne bora kutoka katika vyuo hivyo zilipewa fursa ya kuwasilisha mada katika siku hiyo maalumu ya Utafiti na Ubunifu.

Kutokana na michango na maoni ya wadau ilibainika kuwa Kikao hiki ni muhimu kikiwa kinafanyika kila mwaka kwa kuwa kinatoa fursa ya kuwakutanisha wadau wa serikali mtandao na kusaidia kuleta uelewa wa pamoja kuhusu jitihada zinazoendelea na zijazo, kuongeza ushirikiano, kubadilishana uzoefu, na kujadiliana juu changamoto wanazokumbana nazo na njia mbalimbali za kuzitatua. Pia kujadiliana namna ambavyo tafiti na bunifu zinavyoweza kuchangia kuboresha utekelezaji wa Serikali Mtandao kwa ufanisi.

# UTANGULIZI

Wakala ya Serikali Mtandao (eGA) iliandaa Kikao Kazi cha pili cha Serikali Mtandao kilichofanyika kuanzia **Januari 30** hadi **Februari 2, 2019** jijini Dodoma katika ukumbi wa Chuo cha Sayansi ya Kzompyuta, Habari na Mawasiliano ulipo katika Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM).

**2.1 Lengo la Kikao Kazi**

Lengo la Kikao Kazi cha Pili cha Serikali Mtandao 2019 lilikuwa kubadilishana uzoefu; kujenga uwezo; kuongeza uelewa wa pamoja na ushirikiano; kuainisha na kutafuta njia za kutatua changamoto zinazojitokeza katika utekelezaji wa serikali mtandao nchini.

**2.2 Kauli mbiu**

Kikao Kazi hicho kiliongozwa na Kauli mbiu isemayo **"Uwianishaji wa Rasilimali za TEHAMA kwa Maendeleo ya Viwanda" (Harmonization of ICT Resources for Industrial Development)** ambayo inaonesha umuhimu wa kutumia rasilimali za TEHAMA shirikishi kwa kutumia miundombinu na mifumo ya TEHAMA ya pamoja ili kuleta maendeleo ya viwanda nchini.

**2.3 Ukumbi na Tarehe ya Kikao Kazi**

Kikao Kazi cha Pili cha Serikali Mtandao 2019 kilifanyika Jijini Dodoma katika Ukumbi wa Chuo cha Sayansi ya Kompyuta, Habari na Mawasiliano, Chuo Kikuu cha Dodoma kuanzia tarehe 30 Januari hadi 02 Februari, 2019.

**2.4 Washiriki**

Jumla ya washiriki 786 walihudhuria Kikao Kazi cha Pili cha Serikali Mtandao 2019 na waligawanyika katika makundi matatu kama ifuatavyo:

**2.4.1 Kundi la Kwanza 30 - 31/01 – 2019**

Kundi hili lilihusisha Maofisa ambao ndio watekelezaji wa maamuzi mbalimbali kwenye Taasisi zao ambao ni Wakurugenzi wa TEHAMA, Maofisa TEHAMA Waandamizi, Maofisa Utumishi na Utawala, Maofisa Mawasiliano, Maofisa Masoko, Maofisa Mipango, Maofisa Biashara, Maofisa Ardhi, Maofisa Elimu, Maofisa Ugavi, Maofisa Uhusiano, Maofisa Ununuzi, Maofisa Mipango na Watumiaji Mifumo ya TEHAMA.

### 2.4.2 Kundi la Pili 01 Februari 2019

Kundi hili lilihusisha Makatibu Wakuu, Wakuu wa Taasisi za umma na Wakurugenzi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Tawala za Mikoa ambao ndio watoa maamuzi katika taasisi zao.

### 2.4.3 Kundi la Tatu 02 Februari 2019

Kundi hili lilijumuisha washiriki kutoka kundi la kwanza, la pili na washiriki kutoka Vyuo vinavyotoa mafunzo ya Teknolojia. Hii ilikuwa siku maalumu ya utafiti na ubunifu katika eneo la utekelezaji wa Serikali Mtandao.

## 2.5 Ufadhili wa Kikao Kazi

Kikao Kazi cha Pili cha Serikali Mtandao 2019 kilifadhiliwa na National Microfinance Bank (NMB), National Bank of Commerce (NBC), Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA), Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF), Tume ya Sayansi na Technolojia (COSTECH), Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Bohari Kuu ya Dawa (MSD) na Mamlaka ya Usimamizi wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii (SSRA).

## 2.6 Ada ya Ushiriki

Washiriki wa kikao kazi hili walitoa ada ya ushiriki kulingana na ada za makundi. Kundi la kwanza kila mshiriki alilipa kiasi cha shilingi laki nne tu (400,000), kundi la pili laki mbili tu (200,000). Kundi la tatu Wahadhiri walilipa shilingi elfu hamsini(50,000) na Wanachuo walilipa shilingi elfu ishirini tu(20,000) kwa kila mshiriki.

## 2.7 Maonesho

Katika Kikao kazi cha pili cha Serikali Mtandao 2019, Tafiti na Bunifu kumi bora zilizochaguliwa kutoka katika vyuo vikuu mbalimbali zilionyeshwa kuanzia tarehe 30 Januari hadi 02 Februari 2019. Aidha Taasisi zilizochangia (**Kipengele 2.5**) gharama za uendeshaji zilipewa fursa ya kuonyesha huduma zinazotoa kwa umma.

## 2.8 Kamati za Maandalizi ya Kikao Kazi

Kikao Kazi cha Pili cha Serikali Mtandao 2019 kiliandaliwa na kuendeshwa na Kamati mbalimbali zenye wajumbe walioteuliwa kutoka Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wizara Ujenzi,

Uchukuzi na Mawasiliano, Wakala ya Serikali Mtandao na Chuo Kikuu cha Dodoma. Kamati hizo ni pamoja na Kamati ya Fedha na Ununuzi, Ratiba Hotuba na Taarifa, Uratibu na Itifaki na Kamati ya Elimu na Mawasiliano. Kamati zote zilifanya kazi kwa ushirikiano.

# 3.0 UFUNGUZI NA UFUNGAJI

## 3.1 Ufunguzi wa Kikao Kazi Kundi la Kwanza 30/01/2019

Kikao Kazi cha Pili cha Serikali Mtandao 2019 Kundi la Kwanza kilifunguliwa rasmi na Kaimu Katibu Mkuu Ofisi Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Bw. Mick Kiliba kwa niaba ya Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Dkt. Laurean Ndumbaro.

Bw. Kiliba akifungua Kikao Kazi hicho alifafanua kuwa, kuna mafanikio mengi yaliyopatikana kutokana na uwekezaji katika Serikali Mtandao ikiwa ni pamoja na uwekezaji kwenye miundombinu na mifumo ya TEHAMA kama vile Mtandao wa Mawasiliano Serikalini (GovNet), Vituo vya Kitaifa vya kuhifadhi data (Sehemu ya Serikali) Kutenga Masafa ya Intaneti ya Serikali na utengenezaji wa mifumo mbalimbali ya TEHAMA.

Vilevile, alibainisha baadhi ya changamoto zinazokabili taasisi za umma katika kutekeleza jitihada za serikali mtandao kuwa ni kutozingatia miongozo na kanuni za usimamizi wa Serikali Mtandao, upungufu wa wataalamu wa TEHAMA wenye uwezo na ujuzi wa kutosha na msukumo wa kununua mifumo na miundombinu ya TEHAMA kutoka kwa wafanyabiashara na wafadhili. Pia aliongeza kuwa baadhi ya taasisi zinajitihada za kuianzisha na kutumia mifumo na miundombinu ya TEHAMA ya kwake ambayo ingeweza kutumiwa na taasisi zaidi ya moja hivyo kusababisha urudufu.

Hivyo, alizitaka taasisi za umma kutumia sheria, taratibu, kanuni, viwango na miongozo ya Serikali Mtandao ili kuondoa changamoto hiyo. Pia, alizitaka taasisi za umma kuitambulisha mifumo ya serikali mtandao kwa wananchi ili kuwapunguzia gharama mbalimbali na muda za kupata huduma kutoka Serikalini.



*Mkurugenzi Idara ya Ushauri na Uchambuzi Kazi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Bw. Mick Kiliba akifungua rasmi kikao kazi cha Serikali Mtandao kwa niaba ya Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya utumishi wa Umma katika ukumbi wa Chuo cha Sayansi ya Kompyuta, Habari na Mawasiliano uliopo Chuo Kikuu Dodoma.*

**3.2 Ufunguzi wa Kikao Kazi kwa Kundi la Pili: 01/02/2019**

Kikao Kazi cha Serikali Mtandao 2019 kundi la pili kilichowahusisha Maofisa Masuuli kilifunguliwa rasmi na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Dkt. Mary M. Mwanjelwa (Mb). Mhe. Dkt Mwanjelwa alielekeza kuwa kikao kazi hicho kiwe chachu ya kutoa msukumo mpya wa utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao ikiwa ni pamoja na kujenga uwezo wa watumishi; kuimarisha ushirikiano na mawasiliano ndani ya Serikali; kubadilishana uzoefu na kuhamasisha matumizi ya TEHAMA yenye tija katika kuboresha utendaji wa taasisi za umma na utoaji wa huduma kwa umma.

Mhe. Naibu Waziri alizipongeza taasisi za umma ambazo zimefanikiwa kuboresha utendaji kazi na utoaji huduma kwa umma kwa kutumia TEHAMA. Aidha alisema taasisi za Serikali ambazo bado zina kiwango kidogo cha utekelezaji wa Serikali Mtandao, ni vyema zikaongeza juhudi katika matumizi ya TEHAMA katika utekelezaji wa majukumu yao. Alitoa wito kwa taasisi zote




za umma ambazo zina kiwango kidogo cha utekelezaji wa Serikali Mtandao kuchukua hatua za haraka ili kuhakikisha zinatumia fursa zitokanazo na matumizi ya TEHAMA katika kuongeza ufanisi na kuboresha utoaji wa huduma kwa umma. Naibu Waziri pia alilisisitiza kuwa Serikali imeamua kutoa msukumo kwenye masuala ya Serikali Mtandao, hivyo taasisi za umma hazina budi kushirikiana na Wakala ya Serikali Mtandao katika kuhakikisha kuwa na Serikali Mtandao madhubuti.

Vilevile, alifafanua kuwa Serikali imeweka kipaumbele na kutambua matumizi ya TEHAMA katika Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2015/16 - 2020/21) na Sera ya Taifa ya TEHAMA ya mwaka 2016 ili kufikia malengo ya Taifa na hivyo kusisitiza haja ya ongezeko

la matumizi yake katika utendaji wa shughuli za Serikali na zaidi kuimarisha na kuharakisha utoaji wa huduma kwa umma kwa urahisi, kwa ubora, kwa haraka, kwa gharama nafuu.




*Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Dkt. Mary M. Mwanjelwa (Mb) wakati wa Kikao Kazi cha Pili cha Serikali Mtandao Februari 01, 2019.*

### 3.3 Ufungaji wa Kikao Kazi

Kikao Kazi cha Pili cha Serikali Mtandao 2019 kilifungwa rasmi siku ya Jumamosi tarehe 2 Februari 2019 na Mkurugenzi wa Huduma za TEHAMA wa Wakala, Injinia Benedict Ndomba.



Akifunga kikao hicho Injinia Ndomba aliwashukuru Viongozi wa Mijadala, Watoa mada, Wafadhili, Wabunifu, Watafiti na Washiriki wote kwa kushiriki na kuchangia ujuzi, maarifa na uzoefu wao mkubwa katika masuala mbalimbali yanayohusu Serikali Mtandao. Aidha, aliwaomba washiriki kuyazingatia yote waliyopata kutokana na kikao hicho; Kuongeza ushirikiano kati ya Taasisi na Taasisi, Taasisi na Vyuo, Taasisi na Wafanyakazi na Kushirikiana na Wakala katika utekelezaji wa Serikali Mtandao ili kuboresha utendaji kazi na utoaji wa huduma bora kwa umma kwa kutumia TEHAMA.

# 4.0 UWASILISHAJI WA MADA

## 4.1 Kundi la Kwanza 30/01 - 02 /02/2019.

### 4.1.1 Mada I: Utekelezaji wa Serikali Mtandao Nchini

Mada hii iliwasilishwa na Mtendaji Mkuu wa Wakala ya Serikali Mtandao, Dkt. Jabiri Bakari. Mada hii ililenga kuleta uelewa wa pamoja juu ya dhana ya Serikali Mtandao, jitihada mbalimbali za Serikali Mtandao zilizofanyika, zinazoendelea na zilizopangwa kufanyika ndani ya Serikali. Pia Mtendaji Mkuu alieleza kuhusu fursa zilizopo na jinsi ya kunufaika au kuzitumia katikubaini changamoto na namna ya kukabiliana nazo katika utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao. Aidha alitoa mrejesho wa Kikao Kazi cha Kwanza kilichofanyika Agosti 2015 Jijini Arusha.



Mtendaji Mkuu pia alieleza uzoefu wa utekelezaji wa Serikali Mtandao katika utoaji wa huduma kwa umma na umuhimu wa kuwa na rasilimali shirikishi za TEHAMA zinazosaidia kuwa na matumizi sahihi ya TEHAMA kwenye taasisi za umma.

Alifafanua kuwa dunia inabadilika kwa kasi kutoka katika zama za viwanda asilia vilivyotokana na mapinduzi ya viwanda (Industrial Revolution) ya Karne ya 18 kuelekea katika zama za matumizi makubwa ya TEHAMA ambayo yana mchango mkubwa katika kufikia Maendeleo ya Uchumi wa Kati. Lengo kuu likiwa ni kuhakikisha majadiliano yanajikita katika malengo ya Kikao Kazi hicho kwa kuzingatia hatua nne kuu za ukuaji wa serikali mtandao duniani.

### 4.1.2 Mada II: Taarifa ya Utekelezaji wa Serikali Mtandao – Kila Wizara

Katika uwasilishaji wa taarifa za utekelezaji wa serikali Mtandao, Kila Wizara na taasisi zake ilipaswa kuandaa na kuwasilisha taarifa yake katika Kikao Kazi cha pili cha Serikali Mtandao 2019. Taarifa hizo zililenga kuonyesha hatua za utekelezaji wa Serikali Mtandao (mipango mikakati, mifumo na miundombinu ya TEHAMA) katika kila Wizara; faida kwa Serikali na kwa wananchi zilizopatikana kutokana na utekelezaji huo; changamoto zinazojitokeza na mapendekezo ya kutatua changamoto hizo.

Wizara 16 kati ya Wizara 22 ziliwasilisha taarifa wakati wa Kikao Kazi cha pili cha Serikali Mtandao 2019 kuanzia tarehe 30 hadi 31 Januari 2019 katika makundi kama ilivyopangwa katika Ratiba **(Kiambatisho I).** Hata hivyo, Wizara sita (6) hazikuwasilisha taarifa za utekelezaji wa serikali mtandao katika Kikao Kazi kama ilivyoelekezwa. Tathimini ya uwasilishaji wa taarifa hizo kwa kila Wizara imeoneshwa katika**.**

Baada ya uwasilishaji, washiriki walijadiliana nakutoa mapendekezo muhimu yaliyotokana na changamoto walizonazo ambazo zikifanyiwa kazi zitatatua changamoto kubwa zinazojitokeza katika utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao Mapendekezo hayo yaliwasilishwa katika kikao cha kundi la pili tarehe 1/2/2019 kilichohusisha Makatibu Wakuu, Wakuu wa Taasisi na Wakurugenzi wa Halmashauri za Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kutolewa maamuzi na maelekezo.

**Jedwali I: Wizara zilizowasilisha Taarifa**

| Na. | WIZARA |
|---|---|
| 1. | Ofisi ya Rais-Utumishi wa Umma na Utawala Bora |
| 2. | Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| 3. | Ofisi ya Makamu wa Rais |
| 4. | Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Vijana, ajira na Wenye Ulemavu |
| 5. | Ofisi ya Waziri Mkuu Uwekezaji |
| 6. | Wizara ya Fedha na Mipango |
| 7. | Wizara ya Habari, Utamaduni,Sanaa na Michezo |
| 8. | Wizara wa Ujenzi,Uchukuzi na Mawasiliano |
| 9. | Wizara ya Elimu,Sayansi, Teknolojia na Ufundi |
| 10. | Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii Jinsia, Wazee na Watoto |
| 11. | Wizara ya Maji na Umwagiliaji |

| | |
|---|---|
| 12. | Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi |
| 13. | Wizara ya Katiba na Sheria |
| 14. | Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa |
| 15. | Wizara ya Maliasili na Utalii |
| 16. | Wizara ya Viwanda Biashara na Uwezeshaji |

**Jedwali II: Wizara ambazo hazikuwasilisha Taarifa**

| Na. | WIZARA |
|---|---|
| 1. | Wizara ya Nishati |
| 2. | Wizara ya Mifugo na Uvuvi |
| 3. | Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi |
| 4. | Wizara ya Madini |
| 5. | Wizara wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki |
| 6. | Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. |



***Baadhi ya Washiriki wa Kikao Kazi cha Pili cha Serikali Mtandao 2019 wakichangia mada mbalimbali wakati wa Kikao.***

### 4.2 Kundi la Pili 01/02/2019

Kundi la Pili la Kikao Kazi hiki lilihusisha Makatibu wakuu, Wakuu wa Taasisi na Wakurugenzi wa Mamlaka za serikali za mitaaa. Kundi hili lilijadili kwa kina mapendekezo muhimu yaliyowasilishwa kutoka katika kikao kazi cha kundi la kwanza cha tarehe 30 - 31 Januari 2019. Aidha kundi hili lilitoa ushauri wa jinsi ya kutekeleza mapendekezo hayo.



***Katibu Mkuu (Mawasiliano), Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Dkt. Maria Sasabo, Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Hali ya Hewa Dr. Agnes Lawrence Kijazi, Katibu Mtendaji Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi(NEEC) Bi.Beng'i Issa na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) Mhandisi James Kilaba wakizungumza wakati wa Kikao Kazi cha Pili cha Serikali Mtandao.***

### 4.2.1 Maoni na Hoja (Key Issues) zilizojitokeza katika Utekelezaji wa Serikali Mtandao – Kundi la Kwanza

Kundi la pili la Kikao kazi hiki lilihusisha Makatibu wakuu, Wakuu wa Taasisi na Wakurugenzi wa Mamlaka za serikali za mitaaa. Kundi hili lilijadili kwa kina mapendekezo muhimu yaliyowasilishwa kutoka katika kikao kazi cha kundi la kwanza cha tarehe 30 - 31 Januari 2019. Aidha kundi hili lilitoa maelekezo ili yafanyiwe kazi na kufanikisha utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao nchini .

### 4.3 Majadiliano katika Vikundi (Breakout Session)

Katika siku ya tatu ya kikao kazi 1/02/2019, Kundi la kwanza liligawanyika katika makundi manne kama ifuatavyo:

a) Kundi la kwanza lilihusisha washiriki kutoka katika Ofisi ya makamu wa Rais, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi, Wizara ya Maji na Umwagiliaji , Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii Jinsia, Wazee na Watoto, Wizara wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

b) Kundi la Pili lilihusisha Washiriki kutoka Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Kilimo na Chakula , Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Katiba na Sheria.

c) Kundi la tatu lilihusisha washiriki kutoka Wizara ya ya Madini, Wizara ya Nishati, Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Ujenzi Uchukuzi na Mawasiliano na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

d) Kundi la nne lilihusisha washiriki kutoka katika Wakala ya Serikali Mtandao na baadhi ya Maaofisa kutoka taasisi nyingine za umma.

Makundi hayo yalifanya majadiliano na kuandaa taarifa fupi iliyolenga kuangalia changamoto zinazokabili utekelezaji wa jitihada za Serikali mtandao katika sekta zao; Kuaininisha mbinu zitakazotumika kukabiliana na changamoto hizo; Kuangalia fursa zitakazowezesha utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao kwa ufanisi; Kuandaa maeneo ya kipaumbele katika utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao; Kuandaa mpango wa utekelezaji wa

utatuzi wa changamoto za utekelezaji wa Serikali Mtandao. Taarifa hizo ziliwasilishwa kwa kila kundi na zinaonekana katika Kundi la, kundi la pili, kundi la tatu na Kundi la nne.

### 4.5 Kundi laTatu: Siku Maalumu ya Utafiti na Ubunifu wa Serikali Mtandao

Katika siku hii maalumu ya Utafiti na ubunifu, washiriki kutoka vyuo mbalimbali ikiwa ni pamoja na Wanachuo, Wahadhiri na Wadau wengine walishiriki katika siku hii muhimu ya Utafiti na Ubunifu wa Serikali Mtandao iliyofanyika tarehe 2 Februari, 2019. Aidha, washiriki wa kundi la Kwanza na la Pili nao walishiriki.

Lengo la siku hii maalumu ya ubunifu na utafiti ilikuwa kuonesha umuhimu wa utafiti na ubunifu katika serikali mtandao ili kuboresha utoaji wa huduma kwa umma kwa kushirikiana na Vyuo Vikuu na Vyuo vinavyotoa mafunzo ya teknolojia na Taasisi za Utafiti nchini.

Hivyo, katika Kikao Kazi cha Serikali Mtandao 2019, Vyuo Vikuu, Vyuo vinavyotoa mafunzo ya Teknolojia na Taasisi za Utafiti nchini vilialikwa kuwasilisha bunifu na tafiti katika Serikali Mtandao. Jumla ya Tafiti/Bunifu 24 ziliwasilishwa (**Jedwali III**), ambapo Tafiti/Bunifu 10 zilichaguliwa kushiriki maonesho katika Sehemu maalumu iliyotengwa wakati wa kikao kazi hicho. Aidha Tafiti/Bunifu nne **(4)** bora kutoka katika vyuo hivyo zilipewa fursa ya kuwasilisha mada katika siku maalumu ya Utafiti na Ubunifu. Vyuo hivyo ni Chuo Kikuu cha Dodoma(**Tafiti 1**), Chuo Kikuu cha St. Joseph (**Tafiti 2**) na Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Nelson Mandela (**Tafiti 1**).




*Mtendaji Mkuu Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) Mahandisi Peter Ulanga na Mhadhiri Chuo Kikuu cha Dar es Salaam Bi. Khadija Mkocha wakizungumza wakati wa siku ya Utafiti na Ubunifu wa Serikali Mtandao.*

**Jedwali Na.3 Taasisi zilizowasilisha Tafiti /Bunifu**

| Na. | Taasisi | Tafiti/Bunifu |
|---|---|---|
| 1 | University of Dodoma | Tujifunze Learning Content Management System for Primary Schools |
| 2. | University of Dodoma | Mlinde Game App |
| 3. | Nelson Mandela African Institute of Science And Technology | Machine Learning Based Approach to Measure the Quality of Maternal, Neonatal and Child Health in Developing Countries |
| 4. | Mzumbe University | Real Time Monitoring and Evaluation System to Track Performance of Direct Health Facility Financing and Expected Disbursement |
| 5 | St.Joseph University | Infusion Device for Delivering Intravenous Medication to Patients |
| 6 | St.Joseph University | Telecardiology for Rural Health Care |
| 7 | University of Dodoma | Swahili Language Editing Tool to Support Swahil Writers and Learners |
| 8 | University of Dodoma | Industrial Practical Training Management System |
| 9 | Mbeya University of Science and Technology | Open Performance Review and Appraisal Electronic System |
| 10 | Mbeya University of Science and Technology | Electronic Records and Files Tracking System |
| 11 | The Institute of Finance Management | Incident Management System |
| 12 | St.Joseph University | File Tracking System |
| 13 | Mzumbe University | Factors Influencing Access to Electronic Government Information and E-Government Adoption in Selected Districts of Tanzania |
| 14 | Tanzania Institute of Accountancy | Water Pipe Leakage Reporting System |
| 15 | St.Joseph University | Patient Management System for a Hospital |
| 16 | Mbeya University of Science and Technology | Deployment of All Colleges and Secondary Schools Information System to e-GA Data Center Server |
| 17 | Ardhi University | Mobile App - Coordination |
| 18 | Mzumbe University | Online Management of Student Admissions in High Learning Institutions in Tanzania |
| 19 | University of Dar es Salaam Information and Communication Technology Incubator (UDICCTI) | White Paper: Experience of UDICCTI in Supporting Innovation In Tanzania |
| 20 | University of Dar es Salaam Information and Communication Technology Incubator (UDICCTI) | Agro-Lenz App |

| | | |
|---|---|---|
| **21** | University of Dar es Salaam Information and Communication Technology Incubator (UDICCTI) | Kilimo Taarifa App |
| **22** | University of Dar es Salaam Information and Communication Technology Incubator (UDICCTI) | Electronic Money Exchange App |
| **23** | University of Dar es Salaam Information and Communication Technology Incubator (UDICCTI) | Virtual Environment for Project Implementation |
| **24** | University of Dar es Salaam Information and Communication Technology Incubator (UDICCTI) | Android App for Swash Competition |

Aidha washiriki hao pia walijadiliana na kutoa mapendekezo kuhusu umuhimu wa tafiti na bunifu katika kuboresha utekelezaji wa Serikali Mtandao na mchango wake katika maendeleo ya viwanda.

Vilevile, Tafiti/ Bunifu 10 zilizochaguliwa kutoka katika vyuo zilitunikiwa vyeti kutambua mchango wa ushiriki wao na umuhimu watafiti/binifu kwa maendeleo ya TEHAMA Tanzania. Vyeti hivyo vilitolewa na Mtendaji Mkuu wa Wakala ya Serikali Mtandao, Dkt. Jabiri Bakari.







***Jopo la majaji pamoja na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wakati wa manesho Kikao Kazi cha Pili cha Serikali Mtandao 2019.***



***Mtendaji Mkuu wa Wakala ya Serikali Mtandao Dkt. Jabiri Bakari akitoa vyeti vya ushiriki kwa wanafunzi wa vyuo mbalimbali wakati wa siku ya Utafiti na Ubunifu wa Serikali Mtandao.***

# 5.0 MAMBO MUHIMU YA KUJIFUNZA

Pamoja na mafanikio ya kikao hiki, kulikua mambo yaliyojitokeza ya kujifunza kama ifuatavyo:

i) Taarifa zilizowasilishwa zilionesha Wizara na taasisi zake zinatekeleza jitihada za Serikali Mtandao katika kutoa huduma mtandao, ingawa bado kuna changamoto mbalimbali zinazotakiwa kufanyiwa kazi ili kufikia malengo ya Serikali Mtandao.

ii) Katika uwasilishaji wa taarifa, ilionekana kuwa baadhi Wizara hazikuhusisha taasisi zao za kisekta katika taarifa zao. Hivyo, ilishauriwa Wizara zihusishe taasisi zote za kisekta wakati wa uaandaaji na uwasilishaji wa taarifa.

iii) Kwa kuwa vyuo na taasisi nyingi zilizoalikwa hazikuweza kuwasilisha bunifu na tafiti zao kutokana na muda mfupi wa maandalizi. Hivyo ilipendekezwa kuwe na muda wa kutosha wa maandalizi ya bunifu na tafiti zitakazowasilishwa katika vikao kazi vya serikali mtandao vijavyo.

iv) Ili kuongeza ushiriki wa wadau zaidi kutoka katika taasisi mbalimbali, muda wa maandalizi na wigo wa ufadhili uongezwe.

v) Taasisi nyingi hazikuwa na uelewa wa umuhimu wa kuwa na Kituo cha Utafiti na Ubunifu cha Serikali Mtandao. Jitihada zaidi ziongezwe katika kuzihamasisha Taasisi kutumia kituo hiki katika kuboresha mifumo na miundombinu ya Serikali Mtandao.

# HITIMISHO

Serikali ya Tanzania inatambua matumizi ya TEHAMA katika kuboresha utendaji kazi na utoaji wa huduma kwa umma kwa ufanisi. Pia inatambua fusra zinazopatikana kutokana na matumizi ya TEHAMA na mchango wake katika maendeleo ya wananchi kijamii, kisiasa na kiuchumi. Kwa kutambua mchango huo, Wakala ya Serikali Mtandao inaendelea kuongeza juhudi katika kuhakikisha matumizi ya TEHAMA yanaboresha shughuli za Serikali na kuleta tija na ufanisi katika utendaji kazi na utoaji wa huduma kwa umma wakati huo huo ikiongeza jitihada za kuhakikisha usalama wa mifumo, miundombinu na taarifa zilizopo katika mifumo hiyo.

Katika kuendeleza utekelezaji wa juhudi hizo, Wakala iliandaa Kikao Kazi cha Pili cha Serikali Mtandao kilichofanyika kuanzia tarehe 30 Januari hadi tarehe 2 Februari 2019, ambacho kilitoa fursa ya kuwakutanisha wadau wa serikali mtandao na kuleta uelewa wa pamoja, kuongeza ushirikiano, kubadilishana uzoefu, kujadiliana changamoto wanazokumbana nazo na jinsi ya kuzitatua. Pia, wadau wa serikali mtandao walijadiliana jinsi tafiti na bunifu zinavyoweza kuchangia katika kuongeza ufanisi na tija katika utekelezaji wa jitihada za serikali mtandao.

Kutokana na maoni na michango ya wadau ilibainika kuwa vikao hivi ni muhimu katika kufuatilia utekelezaji wa jitihada mbalimbali za serikali mtandao katika taasisi za umma. Hivyo, ni vyema vikafanyika kila mwaka ili kupata taarifa na mrejesho wa utekelezaji huo. Kikao hiki cha mwaka 2019 kimefanyika kwa ufanisi mkubwa kwa kuwakutanisha wadau mbalimbali kutoka katika taasisi za umma na vyuo Vikuu. Katika Kikao cha Tatu kinachotarajiwa kufanyika mwaka 2020 na kinakusudiwa kuwakutanisha wadau wengi zaidi, kupata uwasilishaji wa taarifa za utekelezaji nyingi zaidi na kupanua wigo wa tafiti na bunifu katika serikali mtandao.

# VIAMBATISH0

**Kiambatisho I: Ratiba ya Kikao Kazi cha Pili cha Serikali Mtandao 2019**

**2nd e-GOVERNMENT ANNUAL MEETING 2019**

**30th January 2019**

**PROVISIONAL PROGRAM**

**Theme: Harmonizing ICT Resources towards Industrial Development**

## 1st GROUP: ICT DIRECTORS, HEAD OF ICT, SENIOR ICT, IT OFFICERS AND SYSTEM USERS

**Day One: 30th 2019**

| TIME | ACTIVITY |
|---|---|
| 07:00 - 08:00 | **Registration** |
| 08:00 - 08:15 | **Opening Remarks**<br>**Dr. Jabiri Bakari (CEO – eGA)** |
| 08:45 - 09:10 | **Official Opening**<br>**Guest of Honor: Mick Kiliba - Acting Permanent Secretary PO-PSGG** |
| 09:10 - 09:15 | **Vote of Thanks: Mr. Priscus Kiwango - Director ICTS, POPSM** |
| 09:15 – 10:00 | **Keynote Address ( e-Government Implementation Status)**<br>**Dr. Jabiri Bakari - CEO- eGA**<br>This presentation will share e- Government Implementation experience in providing shared ICT services to facilitate the adoption of ICT across public institutions. It will explore our rationale for providing shared services, the different types of shared services we have deployed, and the various mechanism (business Models we have adopted to sustain the operations of these shared ICT services. |
| 10:00 – 10:30 | **Health Break** |
| | **Session I:**<br>**Chairperson – Eng. Benedict Ndomba (Director of ICT Management - eGA)**<br>**Panelists:**<br>**1. Dr. Florence Rashidi (Lecturer - UDOM-CIVE)**<br>**2. Mr. Baltazar Kibola (Director of ICT - Ministry of Lands, Housing and Human Settlements Development)** |
| 10:30 – 13:30 | **Presentation from Ministries on e-Government Implementation**<br>Summary Presentation of the report from each ministry and its institutions that aims to examine the e-Government implementation status and see the use of e-Services focusing on citizen and user centric perspective, interoperability, implication to the economic and industrialization growth, the challenges faced and the way forward. |
| 10:30 – 10:55 | **President's Office, Public Service Management & Good Governance** (UTUMISHI, PSC, PSRS, PCCB, Ethics Secretariat, RAMD, TASAF etc.) |
| 10:55 – 11:20 | **President's Office, Regional Administration & Local Government Authorities** |
| 11:20 – 11:40 | **Prime Minister's Office** (Parliament, Labour, NEC, Disaster Management, NSSF, WCF etc.) |
| 11:40 – 12:00 | **Vice President's Office** (NEMC, etc) |

| | |
|---|---|
| **12:00 - 12:25** | **Ministry of Finance and Planning** (BOT, TRA, HAZINA, NBS, PSSSF, NAOT, PPRA, GPSA, SSRA, TADB, TIB, TPB, TIRA, NIC, CMSA, DSE, UTT, NBAA, GAMING BOARD, etc.) |
| **12:25 – 13:00** | **Discussion** |
| **13:00 – 14:00** | **Lunch Break** |
| | **Session II:**<br>**Chairperson: Mr. Priscus Kiwango (Director ICT – PO-PSMGG)**<br>**Panelists:**<br>1. **Ms Connie Francis (Director of ICT - TCRA)**<br>2. **Dr. Alex Mongi Lecturer - (UDOM-CIVE)**<br>3. **Mr. Mtani Yangwe (Director of ICT - Ministry of Tourism and Natural Resources)** |
| | **Presentation from Ministries on e-Government Implementation**<br>Summary Presentation of the report from each ministry and its institutions that aims to examine the e-Government implementation status and see the use of e-Services focusing on citizen and user centric perspective, interoperability, implication to the economic and industrialization growth, the challenges faced and the way forward. |
| **14:00 – 14:05** | **NMB** |
| **14:05 – 14:20** | **Ministry of Works, Transportation and Communication** (TPA, ATCL, TRC, TBA, SUMATRA, TMA, ICTC, TCRA, TTCL, TANROADS, TEMESA, ERB, CRB, AQRB, RFB, NCC, UCSAF, TCAA, TAA, TAZARA, MSCL, TASAC, TPC etc.**)** |
| **14:20 – 14:40** | **Ministry of Education, Science and Technology** (NECTA, NACTE, TCU, HESLB, TIE, TEA, ADEM, COSTECH, TAEC, VETA etc.) |
| **14:40 – 15:00** | **Ministry of Health, Community Development, Gender, Elderly and Children** (MSD, TFDA, NIMR, NHIF, MNH, MOI, etc.) |
| **15:00 – 15:20** | **Ministry of Water and Irrigation** (Water Authorities, DDCA etc.) |
| **15:20 – 15:40** | **Ministry of Lands, Housing and Human Settlements Development (**NHC, WHC, NLUPC, NHBRA etc.) |
| **15:40 –16:00** | **Ministry of Justice and Constitutional Affairs** (Judiciary Services, Attorney General, Law Reform Commission, RITA, CHRAGG etc.) |
| **16:00 – 17:00** | **Discussion** |
| **17:00 –17:20** | **Health Break** |
| **17:20– 17:30** | **Closing Annual Meeting Day One** |

2nd e-GOVERNMENT ANNUAL MEETING 2019
30th January 2019
**PROVISIONAL PROGRAM**
**Theme: Harmonizing ICT Resources towards Industrial Development**

## 1st GROUP: ICT DIRECTORS, HEAD OF ICT, SENIOR ICT, IT OFFICERS AND SYSTEM USERS

### Day Two: 31th January, 2019

| TIME | ACTIVITY |
|---|---|
| 07:00 - 08:00 | **Registration** |
| | **Session III:**<br>**Chairperson: Mr. John Sausi (Director of ICT – Ministry of Finance and Planning)**<br>**Panelists:**<br>1. **Dr. Mustafa Mohsin (Lecturer – UDOM-CIVE)**<br>2. **Mr. Sylvan Shayo (Manager Consulting and Advisory - eGA)**<br>3. **Mr. Ismail Mosses (Lecturer – UDSM-CoICT)** |
| | **Presentation from Ministries on e-Government Implementation**<br>Summary Presentation of the report from each ministry and its institutions that aims to examine the e-Government implementation status and see the use of e-Services focusing on citizen and user centric perspective, interoperability, implication to the economic and industrialization growth, the challenges faced and the way forward |
| 08:00 – 08:15 | **Ministry of Agriculture, Food security and Cooperatives** (NFRA, ASA, TSHTDA, TFRA, TCDC, AGITF, Agricultural Boards etc.) |
| 08:15 –08:30 | **Ministry of Livestock and Fisheries** (LITA, TVLA, TALIRI, TFRI, TLRI, TMPR, TDB, TMB etc.) |
| 08:30 –08:45 | **Ministry of Natural Resources and Tourism (**CAWM\, FITI, FTI, NCT, NMT, TANAPA, NCCA, TTB, PWTI, TaFF, TFS, etc.) |
| 08:45 –09:00 | **Ministry of Industry and Trade** (TANTRADE, SIDO, NDC, BRELA, WMA, EPZA, TIRDO, CAMARTEX, TEMDO, FCC, TIC, TBS, COSOTA, WRRB etc.) |
| 09:00 – 09:15 | **Ministry of Energy** (TANESCO, EWURA, TEITI, REA, TPDC, PBPA, PURA, TGDC etc. ) |
| 09:15 – 09:30 | **Ministry of Minerals** (TGC, MRI, GST, STAMICO, Mining Commission **)** |
| 09:30- 09:45 | **Prime Minister's Office- Labor, Youth, Employment and Persons with Disability** |
| 09:45 – 10:30 | **Discussion** |
| 10:30 – 11:00 | **Health Break** |
| | **Session IV:**<br>**Chairperson: Mr. Ibrahim Mahumi (Director of Human Capital Management - PO-PSMGG)**<br>**Panelists:**<br>1. **Dr. Alex Mongi (Lecturer – UDOM-CIVE)**<br>2. **Mr. Erick Kitali (Director ICT - TAMISEMI)**<br>3. **Mr. Abdallah Samizi (Manager Enterprise Architecture and Mobile Service - eGA)** |

| | |
|---|---|
| | **Presentation from Ministries on e-Government Implementation**<br>Summary Presentation of the report from each ministry and its institutions that aims to examine the e-Government implementation status and see the use of e-Services focusing on citizen and user centric perspective, interoperability, implication to the economic and industrialization growth, the challenges faced and the way forward |
| **11:00 – 11:15** | **Ministry of Defense & National Services** |
| **11:15 –11:30** | **Ministry Home Affairs (NIDA, IMMIGRATION, TPF, PRISON, FIRE & RESCUE FORCE etc.)** |
| | **Ministry of Foreign Affairs East Africa and International Relations** |
| **11:45 –12:00** | **Ministry of Information, Culture ,Arts and Sports ( MAELEZO, TBC, TSN, BAKITA, BASATA, TASUBA, BMT, FILM BOARD)** |
| **12:00 – 13:00** | **Discussion** |
| **13:00 – 14:00** | **Lunch Break** |
| | **Session V**<br>**Presenter and Facilitator: Mr. Mulembwa Munaku (Director ICT-Ministry of Communication)** |
| **14:00 - 15:00** | **Presentation of key e-Government implementation issues** |
| | This session highlights key major issues on e-government implementations and the way forward among the practitioners. |
| **15:00 - 16:00** | Resolutions |
| **16:00 – 16:15** | Vote of Thanks: Meeting Participants |
| **16:45 – 17:15** | **Health Break** |
| **17:15** | **Departure** |

**2nd e-GOVERNMENT ANNUAL MEETING 2019**
**1st February 2019**
**PROVISIONAL PROGRAM**
**Theme: Harmonizing ICT Resources for Industrial Development**

## 2nd GROUP: PERMANENT SECRETARIES, CEOs, DIRECTOR GENERALS, LOCAL GOVERNMENT EXECUTIVE DIRECTORS

**Day One: 1st February 2019**

| TIME | ACTIVITY |
|---|---|
| **07:30 - 08:00** | **Registration** |
| **08:00 - 08:20** | **Opening Remarks: Dr. Jabiri Bakari CEO – eGA** |
| **08:20 – 08:25** | **Open Remarks: Acting PS Mick Kiliba** |
| **08:25 – 08:30** | **Welcoming Remarks: Dodoma Regional Commissioner (RC)** |
| **08:30 – 08:45** | **Official Opening: Deputy Minister of State, President's Office, Public Service Management & Good Governance** |
| **08:45 – 09:00** | **Vote of Thanks: PS – (Communication) Dr. Maria Sasabo** |
| **09:00– 10:00** | **e-Government Implementation Status** |
| | This presentation will share e- Government Implementation experience in providing shared ICT services to facilitate the adoption of ICT across public institutions. It will explore our rationale for providing shared services, the different types of shared services we have deployed, and the various mechanism (business Models we have adopted to sustain the operations of these shared ICT services.<br>**Presenter**: Dr. Jabiri Bakari - CEO- eGA |
| **10:00– 10:30** | **Health Break** |
| **Session I: Chairperson – Dr. Maria Sasabo - PS – (Communication)** | |
| **10:30 – 11:30** | Summary of the key issues on e-Government implementation<br>**Presenter: Dr. Jim Yonazi, Deputy PS (Communication) – Ministry of Works, Transport and Communication** |
| **11:30 – 13:00** | **Discussion** |
| **13:00 – 14:00** | **Lunch Break** |
| **14:00 – 14:05** | **NMB** |
| **Session II: Chairperson – Dr. Maria Sasabo - PS – (Communication)** | |
| **14:05 – 15:30** | **Resolutions** |
| **15:30 -15:40** | **Vote of Thanks:** Eng. Dr. Leonard Chamliho – PS - MWTC- Transport |
| **16:10 - 16:30** | **Health Break** |
| **16:30** | **Departure** |

**Sponsored By:**

## 2nd e-GOVERNMENT ANNUAL MEETING 2019
**2nd February 2019**
**PROVISIONAL PROGRAM**
**Theme: Harmonizing ICT Resources towards Industrial Development**

**3rd GROUP: ALL PARTICIPANTS**
**Research and Innovation Day: 2nd February 2019**

| TIME | ACTIVITY |
|---|---|
| **07:30 - 08:00** | **Registration** |
| **08:00 - 08:30** | **Opening Remarks: CEO – eGA** |
| **08:30 – 08:40** | **Vote of Thanks: Director ICT Management Services - eGA** |
| | **Session I:**<br>**Chairperson: Eng. Peter Ulanga (CEO- UCSAF)**<br>**(Harnessing e-Government Research and Innovation in improving Public Service Delivery)** |
| **08:40– 09:10** | **Research and Innovation on e-Government -** CEO –eGA |
| **09:10– 09:30** | **Research and Innovation on ICT** –-Principal -College of Informatics and Virtual Education UDOM (CIVE) |
| **09: 30 – 09:50** | **Research and Innovation on ICT** – Principal -College of Information and Communication Technologies UDSM (COICT) |
| **09:50 – 10:10** | **Research and Innovation on ICT** – DG – COSTECH |
| **10:10 – 11:00** | **Discussion** |
| **11:00– 11:30** | **Health Break** |
| | **Session II:**<br>**Chairperson: Dr. Amos Nungu (DG – COSTECH)**<br>**(Presentations of Papers Questions and Answers)** |
| **11:30 – 12:00** | Research and Innovation– Paper 1 |
| **12:00- 12:30** | Research and Innovation– Paper 2 |
| **12:30- 13:00** | Research and Innovation– Paper 3 |
| **13:00- 13:30** | Research and Innovation– Paper 4 |
| **13:30 – 14:30** | **Lunch** |
| | **Session III: Facilitators**<br>**Eng. Peter Ulanga (CEO- UCSAF) and**<br>**Dr. Elias Mturi (Deputy Director – University Computing Centre)** |
| **14:30 – 16:00** | **Discussion on the future of e-Government Research and Innovation** |
| **16:00 – 16:30** | **Recognition of the Best Research and Innovation Paper: Dr. Jabiri Bakari (CEO – eGA)** |
| **16:30 -16:40** | **Vote of Thanks: Director ICT Management Services - eGA** |
| **16:40 – 17:00** | **Health Break and Departure** |

## Kiambatishi II: Hotuba

**HOTUBA YA NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS-MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA, MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA (MB), KWENYE UFUNGUZI WA KIKAO KAZI CHA PILI CHA SERIKALI MTANDAO, KUNDI LA PILI KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA CHUO CHA SAYANSI YA KOMPYUTA, HABARI NA MAWASILIANO, CHUO KIKUU CHA DODOMA – DODOMA, TAREHE 01 FEBRUARI, 2019**

---

***Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa, Dkt. Binilith Satano Mahenge;***
***Kaimu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dodoma,***
***Maofisa Masuuli wa Serikali Kuu na Mamlaka za Serikali za Mitaa;***
***Mtendaji Mkuu wa Wakala ya Serikali Mtandao, Dkt. Jabiri Kuwe Bakari;***
***Watendaji Wakuu wa Taasisi za Serikali;***
***Watoa Mada;***
***Wageni Waalikwa;***
***Wana Habari;***
***Mabibi na Mabwana.***

*Habari za Asubuhi.*

Ninapenda kuwashukuru wote waliohusika katika kuandaa Kikao Kazi hiki muhimu na cha pili cha aina yake. Kipekee nawashukuru Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Dkt. Laurean Ndumbaro, Naibu Katibu Mkuu, Dkt. Francis Michael, Mtendaji Mkuu wa Wakala ya Serikali Mtandao Dkt. Jabiri Bakari, pamoja na watumishi walio chini yao kwa maandalizi haya na kwa kunialika kujumuika nanyi kwa ajili ya ufunguzi.

Ninapenda kutambua mchango wa wadau mbalimbali ambao wamefanikisha Kikao Kazi hiki. Michango yenu ya hali na mali imefanikisha kufanyika kwa tukio hili la pili kwenye Utumishi wa Umma. Kipekee ninaomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Benki ya NMB, Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA), Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF), Tume ya Sayansi na Technolojia (COSTECH), Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), Shirika la Hifadhi ya Jamii (NSSF) Bohari Kuu ya Madawa (MSD) na Mamlaka ya Usimamizi wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii (SSRA) ambao wamefadhili Kikao Kazi hiki. Ninawaomba muendelee kuona umuhimu wa kusaidia tena jitihada kama hizi kwa vipindi vijavyo.

Aidha, nawashukuru watoa mada wote, kwa kukubali kujumuika nasi kwa ajili ya kuchangia ujuzi, maarifa na uzoefu wao mkubwa katika masuala mbalimbali yanayohusu Serikali Mtandao. Pia, nawashukuru washiriki wengine wote kwa kukubali kuacha kazi zao nyingine muhimu ili kujumuika nasi kwenye Kikao Kazi hiki kwa lengo la kubadilishana uzoefu, kujenga uelewa wa pamoja na kuendeleza uhusiano katika utendaji kazi na wadau mbalimbali wa Serikali Mtandao. Hivyo, tuna fursa kubwa ya kujifunza mengi miongoni mwetu kwenye eneo hili la Serikali Mtandao. **Karibuni sana.**

***Ndugu Washiriki na Wageni Waalikwa,***

Nimejulishwa kuwa Kikao Kazi hiki kimehudhuriwa na Maofisa Masuuli wa Serikali Kuu na wa Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na Watendaji Wakuu, Wakurugenzi Wakuu wa Taasisi za Umma, ambao ndio watoa maamuzi kwenye Taasisi husika. Nafahamu pia kuwa, Kikao Kazi hiki kimefuatia Kikao Kazi cha aina hii kilichofanyika kwa siku mbili zilizopita na kuwahusisha Maofisa Watendaji wakiwemo Maofisa TEHAMA, Maofisa Ununuzi, Maofisa Mawasiliano Serikalini, Maofisa Utumishi, Maofisa Utawala, Wakaguzi, Wahandisi, Wahasibu, Maofisa Mipango na Watumiaji Mifumo ya TEHAMA ambao ndiyo watekelezaji wa maamuzi mbalimbali kwenye Taasisi zao.

Matarajio yangu ni kuwa, Kikao Kazi hiki kitakuwa chachu ya kutoa msukumo mpya wa utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao, ikiwemo kujenga uwezo ndani ya Serikali na Taasisi zake na kujenga ushirikiano na kuleta uelewa wa pamoja. Aidha, Kikao Kazi hiki ni moja ya mikakati ya kujenga na kuboresha uwezo pamoja na kuimarisha mawasiliano miongoni mwa wadau wa Serikali Mtandao. Pia, kubadilishana uzoefu na kuhamasisha matumizi ya TEHAMA yenye tija katika kuboresha utendaji wa Taasisi za umma ili kutatua changamoto za utendaji.

***Ndugu Washiriki,***

Kikao Kazi hiki kinaongozwa na kauli mbiu isemayo (kwa tafsiri isiyo rasmi) "***Uwianishaji wa Rasilimali za TEHAMA kwa Maendeleo ya Viwanda" ("Harmonization of ICT Resources for Industrial Development").*** Kauli mbiu hii inalenga kuonesha umuhimu na nafasi ya TEHAMA, hususan uwianishaji wa rasilimali za TEHAMA na mchango wake katika wa maendeleo ya viwanda nchini. Niwaombe, kwa umuhimu wa kipekee, mijadala yenu ijikite katika kauli mbiu hii.

***Ndugu Washiriki,***

Dhana ya Serikali Mtandao na utekelezaji wake siyo mpya katika nchi yetu. Kwa ufupi, Serikali Mtandao ni matumizi ya Teknolojia za Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika utendaji kazi Serikalini kwa lengo la kuongeza ufanisi, kupunguza gharama za utendaji na kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi. Serikali Mtandao siyo teknolojia kama inavyochukuliwa na wengi, bali ni matumizi ya TEHAMA katika kuboresha utendaji kazi wa kila siku. Kwa muda sasa, Serikali imetambua umuhimu wa kuboresha huduma zake kwa Umma kupitia matumizi ya TEHAMA, na hivyo kuendelea kuijumuisha katika mipango yake mbalimbali. Aidha, Mipango ya Taifa ya Maendeleo ikiwemo Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025 na Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2015/16 – 2020/21) inatambua nafasi ya TEHAMA katika kufikia malengo ya Taifa na hivyo kusisitiza haja ya ongezeko la matumizi yake katika utendaji wa shughuli za Serikali na utoaji huduma kwa wananchi.

Pamoja na mambo mengine, Sera ya taifa ya TEHAMA ya mwaka 2003 (iliyohuishwa 2016), ilisisitiza juu ya Serikali kutumia fursa zitokanazo na TEHAMA katika kujiendesha na kutoa huduma kwa wananachi. Katika utekelezaji wa Sera hiyo, Serikali iliamua kuanza utekelezaji wa Serikali Mtandao kupitia Mkutano wa Baraza la Mawaziri Na.3/2004 wa tarehe 20 Aprili, 2004 ambapo pamoja na mambo mengine, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma iliagizwa kusimamia na kuratibu uanzishwaji wa Serikali Mtandao. Utekelezaji wa uamuzi huu ulifuatiwa na kuandaliwa kwa Mkakati wa Utekelezaji wa Serikali Mtandao nchini (Julai, 2013), ambao ulilenga

kuhakikisha kuwa uwekezaji na utumiaji wa TEHAMA katika Utumishi wa Umma unakuwa wa manufaa kwa taifa na pia kutoa mwongozo thabiti kuhusu jinsi ya kutekeleza mifumo na mipango ya Serikali Mtandao ambayo hatimaye itasaidia kuimarisha na kuharakisha utoaji wa huduma bora, kwa haraka, kwa gharama nafuu na kwa urahisi.

***Ndugu Washiriki,***

Ili kuhakikisha TEHAMA inatoa mchango chanya katika uendeshaji na usimamizi wa majukumu ya Serikali, jitihada mbalimbali zimefanyika na mafanikio yamepatikana katika maeneo ya sera, sheria, kanuni, miongozo, viwango, mikakati, usalama, miundombinu na mifumo. *Naamini sote tumeona manufaa na* hatua za kuridhisha katika utekelezaji wa Serikali Mtandao. Mafanikio mahususi yaliyopatikana ni pamoja na;

i. Kuanzishwa kwa Wakala ya Serikali Mtandao (*eGA*) ili kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Serikali Mtandao na pia kutoa msaada wa kiufundi, mafunzo na ushauri wa kitaalam kwa Taasisi za Umma.

ii. Kuboreshwa kwa Sera ya TEHAMA 2003 na Mpango Mkakati wa Kitaifa wa Serikali Mtandao, 2013 (*National e-Government Strategy*); kutungwa kwa Sheria za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta, 2010 (*Electronic and Postal Communications, 2010)*, Miamala ya Kielektroniki, 2015 (*Electronic Transactions Act, 2015*); Makosa ya Mitandao, 2015 (*Cybercrimes Act, 2015*); na Sheria ya Serikali Mtandao (*e-Government Act*) ambayo ipo katika hatua za mwisho za maandalizi.

iii. Uwekezaji kwenye miundombinu ya TEHAMA, kama vile Mkongo wa Taifa (*NICTBB*), Mtandao wa Mawasiliano Serikalini (*GovNet*), Vituo vya Kitaifa vya Data (*National Data Centres*), na Masafa ya Intaneti ya Serikali (*Government Internet Bandwidth*);

iv. Kusanifu, kutengeneza, kusimika na kuendesha mifumo mhimili na tumizi ya kimkakati na kisekta kama vile Mfumo wa Rasilimali Watu Serikalini (HCMIS), Mfumo wa Kielektroniki wa Malipo Serikalini (GePG), Mfumo wa Uendeshaji wa Hospitali (GoT-HOMIS), Mfumo wa Manunuzi Serikalini (e-Procurement) na Mfumo wa Uendeshaji wa Masijala Serikalini (e-Office), na

v. Kuongeza njia mbadala za kutolea huduma kwa wananchi kwa kutumia TEHAMA, zikiwemo Tovuti Kuu ya Serikali na Tovuti za Taasisi za Umma, simu za mikononi na vifaa vingine vya kielektroniki.

Kwa ujumla wake, utekelezaji wa juhudi za Serikali Mtandao umechangia kwa kiasi kikubwa katika kurahisisha utoaji wa taarifa na huduma kwa wananchi kwa haraka, uwazi, urahisi, gharama nafuu, zinazopatikana wakati wowote na mahali popote nchini, na duniani kote.

***Ndugu Washiriki,***

Napenda kutumia fursa hii kuzipongeza taasisi za umma ambazo zimefanikiwa kuboresha utendaji kazi na kutoa huduma kwa umma kwa kutumia TEHAMA. Kwa upande wa taasisi za Serikali ambazo bado zina kiwango kidogo cha utekelezaji wa Serikali Mtandao, ni vyema zikaongeza juhudi katika matumizi ya TEHAMA katika

utekelezaji wa majukumu yao. Chukueni hatua za haraka ili kuhakikisha mnatumia fursa zitokanazo na matumizi ya TEHAMA zitakazosaidia kuongeza ufanisi na kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi. Shirikianeni baina yenu na pia shirikianeni na Wakala ya eGA ili tuwe na Serikali Mtandao madhubuti. Serikali itaendelea kutoa msukumo kwenye jambo hili.

***Ndugu Washiriki,***

Pamoja na mafanikio tuliyoyapata, ni vyema tukaendelea kukumbushana kwamba eneo hili bado linakabiliwa na changamoto kadhaa za kiutekelezaji, zikiwemo:

i. Kutokuwepo kwa uwiano wa kutosha kati ya taratibu za utendaji kazi Serikalini (business processes) na teknolojia inayotumika;
ii. Kutokupata thamani halisi ya fedha zinazotolewa kwenye miradi ya TEHAMA Serikalini;
iii. Kuwepo kwa mifumo isiyowasiliana au kubadilishana taarifa (*ndani ya taasisi, na kati ya taasisi na taasisi*);
iv. Urudufu wa mifumo miongoni mwa Taasisi za Serikali yenye viwango na gharama tofauti zisizo na uhalisia;
v. Utegemezi wa wakandarasi kwa kiasi kikubwa katika kushauri, kubuni, kusimamia, kuendesha na kuhifadhi mifumo ya TEHAMA ya Serikali;
vi. Uhusiano na uratibu hafifu wa shughuli za TEHAMA ndani na kati ya Taasisi za Serikali;
vii. Uhaba wa njia za kutosha za kutoa huduma za Serikali Mtandao (*service delivery channels)* ili huduma hizo ziweze kuwafikia wananchi wote hadi vijijini, na pia wenye mahitaji maalum;
viii. Idadi ndogo ya huduma na taarifa za Serikali zinazotolewa kupitia TEHAMA; na
ix. Kuongezeka kwa matishio ya usalama wa taarifa katika mifumo na Miundombinu ya TEHAMA.

***Ndugu Washiriki,***

Tunahitaji kuongeza msukumo ili kupata ufumbuzi wa changamoto hizi kama vile kuwa na sera na sheria mahsusi kwa ajili ya kusimamia utekelezaji wa Serikali Mtandao ili kuziwezesha Taasisi za Serikali kuwa na muono na malengo yanayoshabihiana katika matumizi ya TEHAMA. Vilevile, tunahitaji kuwekeza zaidi ili kuzijengea uwezo Taasisi za Umma na kupata watumishi wenye ujuzi na weledi wa kiwango kinachohitajika ili kukidhi mahitaji ya utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao. Aidha, Serikali imeweka msukumo mpya katika kutekeleza Serikali Mtandao kwa kusisitiza ushirikiano na matumizi ya pamoja ya rasilimali za TEHAMA miongoni mwa taasisi za umma, kutoa miongozo na viwango mbalimbali vya kufuatwa katika utekelezaji wa Serikali Mtandao. Pia, Serikali imedhamiria kuimarisha miundombinu ya TEHAMA, uratibu wa shughuli za TEHAMA na usalama wa taarifa za Serikali. Haya na mengine mengi, yana lengo la kuongeza ufanisi katika Sekta ya Umma, kupunguza gharama za uendeshaji wa shughuli za Serikali na kupanua wigo wa upatikanaji na ubora wa huduma kwa wananchi.

Kwa nafasi zenu kama viongozi na watendaji wakuu wa taasisi, ni lazima kuweka na kutekeleza mikakati kabambe ya namna ya kuzishughulikia changamoto hizi. Nafahamu kwamba changamoto nyingine zinahitaji jitihada za muda mrefu na mtambuka, umiliki wa pamoja wa jitihada hizo, na uelewa wa pamoja kuhusu malengo ya Serikali Mtandao. Hata hivyo, kuna mambo ambayo yapo ndani ya uwezo wa kila

taasisi, hivyo yaanze kufanyiwa kazi haraka ikiwemo kuhakikisha uzingatiaji wa sheria, kanuni, viwango, taratibu na miongozo ya Serikali Mtandao.

***Ndugu Washiriki,***

Kwa namna ya pekee napenda kutoa msisitizo mahsusi kuhusiana na changamoto zinazohusiana na suala la usalama mitandaoni, ambalo bila kukabiliwa kikamilifu, litaathiri kwa kiasi kikubwa jitihada zilizokwishafanyika katika eneo la Serikali Mtandao. Tatizo la usalama mitandaoni linazidi kukua kadri maendeleo ya Teknolojia yanavyozidi kukua. Kwa ajili hiyo, naziagiza taasisi zote za umma kuzingatia viwango vyote vya usalama kwenye mifumo husika katika utekelezaji wa Serikali Mtandao. Usalama wa taarifa za Serikali liwe jambo la lazima wakati wa kubuni, kusanifu, kujenga, kusimika na kuendesha mifumo ya TEHAMA, badala ya kujenga mfumo kwanza na unapokamilika ndipo masuala ya usalama wa mifumo ya TEHAMA yanafikiriwa. Aidha, kama njia mojawapo ya kujihakikishia usalama, utengenezaji wa mifumo yetu uzingatie programu ambazo watalaam wetu wanaweza wakatambua kinachofanyika badala ya kuwa na mifumo ambayo hatujui kinachoendelea nyuma ya pazia.

***Ndugu Washiriki,***

Mafanikio yanayotarajiwa yatafikiwa iwapo kila taasisi ya Serikali itakuwa na watalaam wa kutosha na wenye weledi. Hivyo, nawataka watendaji wakuu wote wa Taasisi za Serikali kuhakikisha mnaimarisha idara na vitengo vya TEHAMA kwa kuwa na watalaam wenye weledi, vitendea kazi vya kutosha na muundo wa usimamizi unaokubalika. Pia, kutokana na mabadiliko ya teknolojia yanayotokea mara kwa mara, taasisi zote zihakikishe zinawajengea watumishi wa TEHAMA uwezo wa kitalaam ili kuendana na kasi hii vinginevyo mafanikio yaliyokwishapatikana yanaweza yasiwe na tija au tusiweze kufikia malengo ya kuhakikisha TEHAMA inatusaidia katika kutekeleza majukumu yetu na kutoa huduma kwa wananchi.

***Ndugu Washiriki,***

Napenda kuwakumbusha na kuwasisitizia kuwa jukumu kubwa la Wakala ya Serikali Mtandao ni kuratibu matumizi ya TEHAMA katika Utumishi wa Umma. Hivyo, ni lazima, Taasisi zote za Umma zishirikiane na Wakala kila zinapobuni na kutekeleza miradi ya TEHAMA. Hii itasaidia kuondoa urudufu wa miradi ya TEHAMA miongoni mwa taasisi za Serikali. Hatuwezi kuendelea kufanya kama tulivyofanya hapo awali kabla ya kuanzisha Wakala. Ni ukweli usiopingika kwamba hakuna sekta yoyote iliyoendelea bila kuratibiwa, kwa hiyo ni vema mkazingatia miongozo mbalimbali inayotolewa katika kutekeleza Serikali Mtandao.

Kwa upande wa Wakala ya Serikali Mtandao, natoa rai mhakikishe mnaendelea kujenga uwezo wa kutosha na kuweka utaratibu mzuri wa kuzisaidia taasisi za Umma katika matumizi ya TEHAMA na kamwe msigeuke kikwazo. Aidha, muendelee kufanya tafiti za Serikali Mtandao ambazo zitazisaidia taasisi za Umma kuboresha utoaji wa huduma. Pia, naipongeza Wakala kwa kuwa na utaratibu wa kubuni, kujenga na kusimamia miundombinu na mifumo shirikishi ya TEHAMA ambayo inasaidia utekelezaji wa Serikali Mtandao katika Taasisi za Umma.

***Ndugu Washiriki,***

Kama kauli mbiu yetu inavyotuambia, maendeleo ya viwanda nchini yanategemea pamoja na mambo mengine uwezeshaji wa TEHAMA ambayo pia inasaidia upatikanaji wa taarifa sahihi na kwa wakati ili kusaidia kufanya maamuzi sahihi na kwa haraka, na kuwawezesha wananchi kupata huduma mbalimbali kama vile uanzishaji wa biashara, uombaji wa vibali mbalimbali na huduma ambazo zinahusiana na shughuli za kiuchumi za wananchi. Hivyo, mtakubaliana na mimi kwamba, iwapo utekelezaji wa mifumo na miundombinu ya TEHAMA utawianishwa na kuwezesha ubadilishanaji wa taarifa ndani ya taasisi za umma na baina ya taasisi za umma, utoaji wa huduma kwa njia ya mtandao utakuwa ni kichocheo muhimu katika kufikia maendeleo ya viwanda tunayokusudia kuyapata. Hivyo, Taasisi zote za Umma zihakikishe zinazingatia Sheria, Kanuni, Taratibu, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao iliyowekwa na inayoendelea kuwekwa ili kuhakikisha matumizi sahihi ya TEHAMA ndani ya Utumishi wa Umma.

***Ndugu Washiriki,***

Namalizia kwa kuwakumbusha kwamba utekelezaji wa Serikali Mtandao unahitaji jitihada na utashi wa pamoja wa viongozi, watendaji, wananchi na wadau wengine. Serikali imeweka mazingira mazuri ya kisera, kisheria na kimkakati ili kuhakikisha kuwa matumizi ya TEHAMA yanakuwa na tija katika kuwahudumia wananchi na kuwaondolea kero mbalimbali.

Hivyo, niwaombe mtumie siku hii ya leo ya Kikao Kazi hiki, kusikiliza kwa umakini mada mbalimbali na kushiriki kikamilifu mijadala itakayofuata kwa umakini na uwazi ili hatimaye mtoke na mapendekezo yatakayowezesha Serikali kufanya utoaji wa huduma kwa Umma kupitia TEHAMA uwe bora zaidi, wenye ufanisi, na unaokidhi matarajio ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Mwisho, natarajia kuwa Kikao Kazi hiki kitakuwa chachu ya kuanza maandalizi ya Kikao Kazi kingine kwa mwaka ujao. Ni vyema kuhakikisha kuwa ubadilishanaji wetu wa uzoefu kupitia majadiliano na kuelimishana unakuwa endelevu. Na, ni muhimu kila mmoja wenu aendelee kushiriki pale mtakapotaarifiwa.

Baada ya kusema hayo sasa natamka kwamba Kikao Kazi cha Mwaka 2019 cha Serikali Mtandao, Kundi la Pili, kimefunguliwa rasmi.

*Asanteni kwa kunisikiliza.*

**HOTUBA YA KATIBU MKUU, OFISI YA RAIS-MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA DKT. LAUREAN NDUMBARO KWENYE UFUNGUZI WA KIKAO KAZI CHA PILI CHA SERIKALI MTANDAO, KUNDI LA KWANZA, KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA CHUO CHA SAYANSI YA KOMPYUTA, HABARI NA MAWASILIANO, CHUO KIKUU CHA DODOMA – DODOMA,**
**TAREHE 30 - 31 JANUARI, 2019**

---

***Mtendaji Mkuu wa Wakala ya Serikali Mtandao,***
***Watendaji wa Taasisi za Serikali,***
***Watoa Mada,***
***Wageni Waalikwa,***
***Wana Habari,***
***Mabibi na Mabwana,***

***Habari za asubuhi.***

Awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujalia uzima, afya na nguvu za kutuwezesha kuwepo hapa leo hii. Aidha, napenda kuwashukuru waandaaji kwa kufanikisha kuwepo kwa Kikao Kazi cha Pili cha Serikali Mtandao na pia kwa kunipa heshima ya kuwa mgeni rasmi katika tukio la ufunguzi wake.

Pia, nachukua fursa hii kuwakaribisha washiriki wote wa Kikao Kazi hiki kwa Kundi la Kwanza linalojumuisha Maofisa Watendaji wakiwemo, Maofisa TEHAMA, Maofisa Ununuzi, Maofisa Mawasiliano Serikalini, Maofisa Utumishi, Maofisa Utawala, Wakaguzi, Wahandisi, Wahasibu, Maofisa Mipango na Watumiaji Mifumo ya TEHAMA. Nawakaribisha pia wadau mbalimbali ambao mmeona umuhimu wa kuhudhuria tukio hili muhimu katika jitihada zetu za kujengeana uwezo, kujenga ushirikiano na kupata uelewa wa pamoja juu ya utekelezaji wa Serikali Mtandao kwenye Utumishi wa Umma.

Ninapenda kutambua mchango wa wadau mbalimbali ambao wamefanikisha Kikao Kazi hiki cha Pili. Michango yenu ya hali na mali imewezesha kufanyika kwa tukio hili muhimu kwenye Utumishi wa Umma. Kipekee ninaomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Benki ya NMB, Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA), Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF), Tume ya Sayansi na Technolojia (COSTECH), Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), Shirika la Hifadhi ya Jamii (NSSF), Bohari Kuu ya Madawa (MSD) na Mamlaka ya Usimamizi wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii (SSRA) ambao mmefadhili Kikao Kazi hiki. Ninawaomba muendelee kusaidia jitihada hizi kwa vipindi vijavyo.

Kwa umuhimu wa pekee, naipongeza Wakala ya Serikali Mtandao kwa kuendelea kuwa wabunifu wa masuala mbalimbali yanayohusu Serikali Mtandao ikiwemo uandaaji wa tukio hili kwa mara ya pili.

***Ndugu Washiriki,***

Kikao Kazi hiki kinalenga kuwakutanisha wadau wanaohusika na utekelezaji wa Serikali Mtandao kwa ajili ya kujenga uwezo, kuongeza ushirikiano na kubadilishana uzoefu. Aidha, malengo mengine ya Kikao Kazi hiki ni kujadiliana njia sahihi za kukabiliana na changamoto zinazojitokeza katika jitihada mbalimbali za utekelezaji wa Serikali Mtandao. Hivyo, mada zote zitakazojadiliwa katika Kikao Kazi

hiki zitajikita katika maeneo hayo. Pamoja na mada hizo, pia mtapata fursa ya kujadili, kutoa maoni na mapendekezo yenye lengo la kuboresha zaidi utekelezaji wa Serikali Mtandao.

***Ndugu Washiriki,***

Kikao Kazi hiki kinaongozwa na kauli mbiu isemayo (kwa tafsiri isiyo rasmi) "***Uwianishaji wa Rasilimali za TEHAMA kwa Maendeleo ya Viwanda" ("Harmonization of ICT Resources for Industrial Development").*** Kauli mbiu hii inalenga kuonesha umuhimu na nafasi ya TEHAMA, hususan uwianishaji wa rasilimali za TEHAMA na mchango wake katika maendeleo ya viwanda nchini. Ni rai yangu kwamba, kwa umuhimu wa kipekee, mijadala yenu pia ijikite na kujielekeza katika kauli mbiu hii.

***Ndugu washiriki,***

Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ndiyo yenye dhamana ya kusimamia utekelezaji wa Serikali Mtandao. Hii inatokana na dhamana ya Wizara hii iliyopewa ya kusimamia Utumishi wa Umma. Msingi mkuu wa Utumishi wa Umma ni ubora wa huduma zinazotolewa na taasisi za umma kwa wananchi. Hivyo, maboresho ya Utumishi wa Umma yamefanyika pia katika eneo la sera na mifumo ya kusaidia utendaji kazi (policies and systems to support service delivery) kwa lengo la kuwa na mikakati ya kisera na kimfumo ya kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi.

***Ndugu washiriki,***

Utekelezaji wa Serikali Mtandao ni moja ya sehemu muhimu ya maboresho yaliyofanyika katika Utumishi wa Umma, ambao umesaidia kurahisisha utoaji wa huduma zinazopatika kwa urahisi na kwa gharama nafuu kwa kutumia TEHAMA. Utekelezaji wa Serikali Mtandao umejikita katika kuboresha utoaji wa huduma miongoni mwa taasisi za umma (Government to Government), kati ya taasisi za umma na wananchi (Government to Citizens), kati ya taasisi za umma na sekta ya Biashara (Government to Business), na kwa Serikali kuwahudumia watumishi (Government to Employees).

***Ndugu washiriki,***

Napenda kuipongeza Wakala ya Serikali Mtandao kwa mafanikio yaliyopatikana hadi sasa katika shughuli zake za utekelezaji wa Serikali Mtandao, hasa kutokana na kutenda kazi kwa weledi, ubunifu, na juhudi kubwa. Mafanikio makubwa yamepatikana katika uratibu, usimamizi, utoaji wa msaada wa kiufundi, mafunzo na ushauri wa kitaalam kwenye Taasisi za Umma ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Serikali Mtandao. Mafanikio mengine yaliyopatikana ni pamoja na:

i. Kusanifu, Kubuni, kusimika na kusimamia uendeshaji wa miundombinu na mifumo mihimili na tumizi ya TEHAMA katika Utumishi wa Umma ikiwemo Mfumo wa Uendeshaji Masijala Serikalini (e-Office), Mfumo wa Barua Pepe Serikalini (GMS), Mfumo wa Vibali vya Safari (e-Vibali), Mfumo wa Usimamizi Rasilimali Watu Serikalini (HCMIS), Mfumo wa Malipo wa Serikali Kielektroniki (GePG), Mfumo wa Uendeshaji wa Hospital (GoT-HOMIS), Mfumo wa Manunuzi Serikalini (e-Procurement) na Vituo vya Serikali vya Kuhifadhi Data (Government Data Centres).

ii. Kutengeneza Miongozo na Viwango vya Serikali Mtandao vinavyotumiwa na Taasisi za Umma katika kusanifu, kutengeneza na kuendesha mifumo na miundombinu ya TEHAMA katika maeneo mbalimbali ya utekelezaji wa Serikali Mtandao.

iii. Kuongeza njia mbadala za kutolea huduma kwa wananchi kwa kutumia TEHAMA, kama vile Tovuti Kuu ya Serikali, Tovuti Kuu ya Ajira, Tovuti mbalimbali za taasisi za umma, simu za mikononi na vifaa vingine vya kielektroniki.

iv. Kushiriki na kutoa mchango wa kitaalam katika maandalizi ya Sheria ya Serikali Mtandao (e-Government Act) ambayo ipo katika hatua za mwisho.

***Ndugu Washiriki,***

Utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao umechangia kwa kiasi kikubwa katika kurahisisha utoaji wa taarifa na huduma nyingine kwa wananchi kwa haraka, uwazi, urahisi, gharama nafuu, wakati wowote na mahali popote nchini, na kwingineko duniani. Hiki ni kichocheo muhimu katika kufikia Dira ya Taifa ya Mwaka 2025 inayolenga, pamoja na mambo mengine, kufikia Maendeleo ya Viwanda.

***Ndugu Washiriki,***

Mafanikio ya Wakala ya Serikali Mtandao yametokana na juhudi zilizofanywa na Serikali katika Sekta ya TEHAMA nchini. Juhudi hizi ni pamoja na uwepo wa Sera, Sheria na Miongozo inayosimamia Sekta ya TEHAMA nchini ambayo imechangia kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa Serikali Mtandao. Vilevile, uwepo wa miundombinu ya TEHAMA nchini imekuwa ni mhimili muhimu katika utoaji wa huduma mbalimbali za Serikali Mtandao. Baadhi ya mafanikio mahususi yaliyochangia ukuaji wa Serikali Mtandao ni pamoja na:

i. Uboreshaji wa sera na sheria, ikiwemo kutungwa kwa Sera ya TEHAMA 2016, na Sheria ya "*Electronic and Postal Communications*" 2010, Sheria za Miamala ya Kielektroniki, 2015 (*Electronic Transactions Act, 2015*); Sheria ya Makosa ya Mitandao, 2015 (*Cybercrimes Act, 2015*);

ii. Kufanyika kwa uwekezaji mkubwa kwenye miundombinu ya TEHAMA, kama vile Mkongo wa Taifa (*NICTBB*), Vituo vya Kitaifa vya Data (*National Data Centres*), na kutenga Masafa ya Intaneti ya Serikali (*Internet Bandwidth*);

***Ndugu Washiriki,***

Pamoja na mafanikio yaliyokwishapatikana, bado kuna changamoto zinazokabili utekelezaji wa Serikali Mtandao. Baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na baadhi ya mifumo ya TEHAMA kuendelea kutowasiliana na kutobadilishana taarifa (ndani ya taasisi, na kati ya taasisi na taasisi), urudufu wa mifumo ambapo kila taasisi inakuwa na juhudi za kipekee katika kusimika na kutumia mifumo na miundombinu ya TEHAMA ambayo ingeweza kutumiwa na zaidi ya taasisi moja na utumiaji wa viwango tofauti katika usanikishaji wa mifumo. Baadhi ya sababu zinazochangia uwepo wa changamoto hizi ni pamoja na kutozingatia miongozo na kanuni za usimamizi wa Serikali Mtandao zilizopo, upungufu wa watalaamu wa TEHAMA wenye

uwezo na ujuzi wa kutosha, misukumo kutoka kwa wafanyabiashara na wafadhili, na uratibu hafifu wa shughuli za TEHAMA ndani na kati ya Taasisi za Serikali. Ni matumaini yangu kuwa, katika Kikao Kazi hiki, mtabadilishana uzoefu kuhusu hatua zinazochukuliwa na zinazoweza kuchukuliwa ili kuwa na kanuni au miongozo ya usimamizi wa mifumo na vifaa vya Serikali Mtandao, ambayo itasaidia, pamoja na mambo mengine, kuboresha mahusiano na uratibu wa shughuli za TEHAMA Serikalini. Pia mtajulishwa changamoto zilizobainishwa katika Kikao Kazi kilichopita pamoja na hatua zilizochukuliwa katika utatuzi wake.

***Ndugu Washiriki,***

Tunafahamu kuwa lengo kuu la utekelezaji wa Serikali Mtandao ni kuboresha utoaji wa huduma kwa umma, lakini pia utekelezaji wake unalenga kuimarisha utawala bora na kuongeza tija na ufanisi katika uendeshaji wa taasisi za Umma kwa kuhakikisha uwepo wa mawasiliano ya haraka, yenye uhakika na salama ndani na kati ya taasisi mbalimbali za Serikali; kuanzia kwenye Wizara, Mikoa hadi ngazi za Halmashauri pamoja, taasisi za umma zinazojitegemea na Balozi zetu nje ya nchi. Aidha, Serikali Mtandao inadhamiria kupunguza gharama za uendeshaji wa Serikali; kupanua wigo wa upatikanaji wa taarifa muhimu katika kila ngazi Serikalini; kuimarisha usalama wa taarifa za Serikali na kuongeza uwezo wa Serikali kupambana na majanga kwa kutumia teknolojia; kurahisisha michakato ya utendaji kazi katika taasisi za Serikali, kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi na kuongeza udhibiti wa mapato ya Serikali.

***Ndugu Washiriki,***

Utekelezaji wa malengo haya unategemea uimara wa mifumo ya uendeshaji katika Utumishi wa Umma. Kukiwa na mifumo dhaifu, uboreshaji wa huduma zetu kwa kutumia TEHAMA utakuwa mgumu. Tukiwa na mifumo imara, matumizi ya TEHAMA yatatusaidia kuleta tija na ufanisi wa utoaji wa huduma zetu. Naomba ikumbukwe kuwa, Serikali ilifanya maboresho ya mifumo ya utendaji kazi (business process improvement) wakati wa Programu ya maboresho ya Utumishi ya Umma (PSRP). Hivyo, ni vyema tukatumia fursa za TEHAMA kuendelea kuboresha mifumo hiyo na pia kufanya mapitio ya mara kwa mara ili kuendelea kuimarisha na kuifanya ilete tija na ufanisi uliokusudiwa kwani maboresho ni zoezi endelevu.

Ni vyema kukumbushana kuwa utekelezaji wa Serikali Mtandao ni suala la kisera na kimkakati. Hivyo ubunifu wa sera na mikakati ya utekelezaji wa Serikali Mtandao itazamwe mara kwa mara kulingana na maendeleo ya kiteknolojia yanayotokea na changamoto zake.

***Ndugu Washiriki,***

Kama kauli mbiu yetu inavyotuambia, ukuaji wa viwanda nchini unategemea pamoja na mambo mengine, uwezeshaji wa TEHAMA ambao unasaidia upatikanaji wa taarifa sahihi na kwa wakati ili kusaidia kufanya maamuzi sahihi na kwa haraka, uwezeshaji wa wananchi kupata huduma mbalimbali kama vile katika uanzishaji wa biashara, uombaji wa vibali mbalimbali na huduma ambazo zinahusiana na shughuli za kiuchumi za wananchi. Mtakubaliana na mimi ya kwamba, iwapo mifumo na miundombinu ya TEHAMA itakuwa imewianishwa na kuwezesha kubadilishana taarifa, itasaidia uboreshajii wa shughuli mbalimbali katika Utumishi wa Umma. Hivyo, ninazisihi Taasisi zote za Umma zihakikishe zinazingatia Sheria, Kanuni, Taratibu, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao iliyowekwa ili kuboresha utendaji wa Serikali utakao rahisisha upatikanaji wa huduma kwa wananchi na hivyo kutuwezesha kuufikia uchumi wa viwanda tunaoutarajia.

***Ndugu Washiriki,***

Kwa kumalizia, nawaomba msikilize kwa makini mada zote zitakazotolewa na kushiriki kikamilifu, katika mijadala na hoja kwa uwazi ili kujenga uelewa wa pamoja kuhusiana na utekelezaji wa Serikali Mtandao. Aidha, niwakumbushe kuwa, ninyi kama watumishi wa umma, ni muhimu kutambua kuwa wakati wote Utumishi wa Umma unaohitajika ni ule wenye maadili, weledi na ubunifu katika utendaji kazi, na siyo wa kufanya kazi kwa mazoea au kwa kusukumwa. Hivyo nawaasa tuwe na mitazamo ya kujiendeleza na kufanya kazi kwa bidii ili tuweze kuwa wabunifu katika kutimiza wajibu wetu wa kila siku. Ni muhimu wote tukatambua kuwa, UTUMISHI WA UMMA IMARA HUJENGA SERIKALI NA TAIFA IMARA, NA KUCHANGIA KATIKA KUFIKIA MAENDELEO YA VIWANDA YANAYOKUSUDIWA.

***Baada ya kusema hayo, sasa napenda kutamka kwamba Kikao Kazi hiki kimefunguliwa rasmi.***

***ASANTENI KWA KUNISIKILIZA***

**NENO LA UKARIBISHO LA MTENDAJI MKUU WA WAKALA YA SERIKALI MTANDAO, DKT. JABIRI BAKARI KWENYE UFUNGUZI WA KIKAO KAZI CHA PILI CHA SERIKALI MTANDAO KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA CHUO CHA SAYANSI YA KOMPYUTA, HABARI NA MAWASILIANO, CHUO KIKUU CHA DODOMA – DODOMA, TAREHE 01 FEBRUARI, 2019**

***Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mh. Dkt. Mary Mwanjelwa (MB);***
***Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa, Dkt. Binilith Satano Mahenge;***
***Kaimu Makamu Mkuu wa Chuo, Kikuu cha Dodoma, Prof. Peter Lawrence Msoffe;***
***Maofisa Masuuli wa Serikali Kuu na Mamlaka za Serikali za Mitaa;***
***Watendaji Wakuu wa Taasisi za Serikali;***
***Mkurugenzi wa Serikali Mtandao Zanzibar;***
***Pia Napenda Kutambua Uwepo wa-***
***Wajumbe kutoka Zanzibar;***
***Wawakilishi Kutoka Vyuo Vikuu vya Dodoma (UDOM), Dar es salaam (UDSM), Nelson Mandela (NM-AIST), St. Joseph (SJUIT), na Mbeya (MUST);***
***Wakurugenzi, Wakuu wa Idara/Vitengo na Maafisa Waandamizi wa TEHAMA Serikalini;***
***Maafisa Ununuzi, Mipango, Mawasiliano, Utumishi, Utawala, Wakaguzi, Wahandisi, na Wahasibu;***
***Watoa Mada;***
***Watumishi wa Ofisi ya Rai, Menejiment ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora;***
***Watumishi wa Chuo Kikuu Cha Dodoma***
***Watumishi wa Wakala ya Serikali Mtandao;***
***Wageni Waalikwa;***
***Wana Habari;***
***Mabibi na Mabwana.***

***Habari za asubuhi.***
***Ndugu Mgeni Rasmi;***

Awali ya yote niaenze kwa kumshukuru Mwenyezi, mwingi wa rehema kwa kutuwezesha kuwa hapa leo hii. Kwa heshima na taadhima, nachukua fursa hii kukukaribisha Ndugu Mgeni Rasmi pamoja na washiriki wote kwenye Awamu ya Pili ya Kikao Kazi cha Pili cha Serikali Mtandao kilichoanza Januari 30, 2019 na kinatarajiwa kumalizika Februari 2, 2019.

***Ndugu Mgeni Rasmi na Washiriki;***
Kikao hiki cha Pili cha Serikali Mtandao, kilianza na Awamu ya Kwanza tarehe 30 na 31 Januari, 2019 ambayo ilihusisha Wakurugenzi wa TEHAMA, Wakuu wa Idara na Vitengo vya TEHAMA Serikalini, Maofisa Waandamizi wa TEHAMA, Maofisa Ununuzi, Maofisa Mawasiliano, Maofisa Utumishi, Maofisa Utawala, Wakaguzi, Wahandisi, Wahasibu, Maofisa Mipango na Watumiaji wa Mifumo ya TEHAMA. Awamu hii ya Pili ambayo tupo nayo hii leo, inahusisha Maofisa Masuuli wa Serikali Kuu na Mamlaka za Serikali za Mitaa na Watendaji Wakuu wa Taasisi za Serikali. Aidha, Awamu ya Tatu ambayo itafanyika kesho, Februari 02, 2019 itahusisha washiriki wote waliojisajili kwa ajili ya Siku ya Utafiti na Ubunifu wa Serikali Mtandao na wadau wengine wa Serikali Mtandao. Kikao Kazi hiki cha Pili cha Serikali Mtandao kina washiriki wapatao 753, ambapo kati ya hawa washiriki 106 ni Maofisa Masuuli na Wakuu wa Taasisi za

Umma, 606 walikuwa ni Wakuu wa Idara/vITENGO vya TEHAMA Serikalini, na wahiriki 41 ni wawakilishi kutoka vyu vikuu,

***Ndugu Mgeni Rasmi na Washiriki;***

Hiki ni *Kikao Kazi cha Pili cha Serikali Mtandao* kufanyika hapa nchini baada ya kile cha Kwanza kilichofanyika Jijini Arusha Mwezi Agosti, 2015. Katika kikao hiki yatawasilishwa yatokanayo na kikao cha kwanza na wajumbe, na watapata fursa ya kujadili utekelezaji wa maazimio yaliyotolewa katika kikao hicho, na pia watajadili hali ya utekelezaji wa Serikali Mtandao katika sekta mbalimbali nchini.

***Ndugu Mgeni Rasmi;***

Katika Awamu ya Kwanza iliyomalizika jana, tulipokea na kujadili ripoti za utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao kutoka katika Wizara mbalimbali na taasisi zake. Awamu ya Tatu itakuwa kesho, ambayo itakuwa siku ya ubunifu na utafiti katika eneo la Serikali Mtandao, ambapo bunifu na tafiti mbalimbali zitaoneshwa. Aidha, wajumbe watapata fursa na kujadiliana maeneo ya utafiti na ubunifu ikiwa ni sehemu ya kutafuta ufumbuzi wa changamoto zilizoibuliwa katika awamu za vikao vilivyopita kwa ajili ya maendeleo ya Serikali Mtandao kwa siku zijazo.

***Ndugu Mgeni Rasmi na Washiriki;***

Kaulimbiu ya Kikao Kazi cha pili cha Serikali Mtandao (Kwa Tafsili isiyo rasmi) ni "***Uwianishaji wa Rasilimali za TEHAMA kwa Maendeleo ya Viwanda*** (***Harmonization of ICT Resources for Industrial Development***). Dhana ya Kaulimbiu hii ni kuhamasishana, kukubaliana, na hatimaye kuwa na uelewa wa pamoja wa namna na umuhimu wa kuwianisha rasilimali za TEHAMA ili iwe chachu ya kuleta maendeleo ya viwanda nchini.

***Ndugu Mgeni Rasmi na Washiriki;***

Ni wazi kuwa, dunia inahama kwa kasi kutoka katika mfumo wa viwanda asilia vilivyotokana na mapinduzi ya viwanda (Industrial Revolution) ya Karne ya 18 kuelekea katika matumizi makubwa ya TEHAMA ambayo yana mchango mkubwa katika kufikia Maendeleo ya Uchumi wa Viwanda. Hali hii inayojulikana kama mapinduzi ya Kidijitali (digital revolution) imetuingiza katika Zama za Taarifa (information Age) ambayo ni mhimili mkubwa katika maendeleo ya viwanda, na katika sekta zote (kilimo, Madni, Utalii, Elimu, Afya, Fedha nk)

***Ndugu Mgeni Rasmi;***

Kipekee nichukue fursa hii kutoa shukrani za pekee kwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa msaada wa hali na mali uliowezesha kufanikisha Kikao Kazi hiki muhimu. Shukrani nyingne ziende kwa Wafanyakani Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), wafanyakazi wa wenzangu wa Wakala ya Swrikali Mtandao na wale wa taasisi nyingine, Wafanyakazi wa Chuo Kikuu cha Dodoma husun wa College of Informatics and Virtual Education) Mwisho, japo si kwa umuhimu, naomba nitambue michango ya hali na mali kutoka kwa wadau wetu wote waliowezesha kufanyika kwa Kikao Kazi hiki. Wadau hao ni taasisi za Serikali zilizo changia kwa kuleta wawakilishi. Kipekee napenda kutoa shukrani za dhati kwa taasisi zilizo fadhili Kikao Kazi hiki, ambazo ni Benki ya NMB, Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA),

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF), Tume ya Sayansi na Technolojia (COSTECH), Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), Shirika la Hifadhi ya Jamii (NSSF) Bohari Kuu ya Madawa (MSD) na Mamlaka ya Usimamizi wa Mifuko ya Hifadhi Jamii (SSRA).

Baada ya kusema hayo, nakushukuru sana mgeni rasmi na washiriki wote kwa kujumuika nasi katika Kikao Kazi Hiki cha Pili cha Serikali Mtandao, na naomba sasa kumkaribisha mratibu wa shughuli hii aendelee na ratiba.

**ASANTENI KWA KUNISIKILIZA.**

**NENO LA SHUKURANI UFUNGAJI WA KIKAO KAZI CHA PILI CHA SERIKALI MTANDAO, KUNDI LA TATU KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA CHUO CHA SAYANSI YA KOMPYUTA, HABARI NA MAWASILIANO, CHUO KIKUU CHA DODOMA – DODOMA, TAREHE 02 FEBRUARI, 2019**

---

***Maofisa Masuuli wa Serikali Kuu na Mamlaka za Serikali za Mitaa;***

***Mtendaji Mkuu Wakala ya Serikali Mtandao, Dkt. Jabiri Bakari;***

***Watendaji Wakuu wa Taasisi za Serikali;***

***Mkurungezi wa Serikali Mtandao Zanzibar; Ndugu Shaban Chum***

***Wawakilishi kutoka Vyuo vya Elimu ya Juu;***

***Watoa Mada;***

***Wageni Waalikwa;***

***Wana Habari;***

***Mabibi na Mabwana.***

***Habarini za Jioni.***

Awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuturuhusu kufika muda huu. Pia nitoe shukrani zangu za dhati kwa kupewa nafasi hii ya kutoa neno la shukrani katika ufungaji wa Awamu ya Tatu ya Kikao Kazi cha Pili cha Serikali Mtandao 2019 chenye kauli mbiu ya **"Uwianishaji wa Rasilimali za TEHAMA kwa Maendeleo ya Viwanda".**

***Ndugu Mwenyekiti,*** ninapenda kuwashukuru Viongozi wote wa Mijadala, Watoa mada wote, kwa kukubali kujumuika nasi kwa ajili ya kuchangia ujuzi, maarifa na uzoefu wao mkubwa katika masuala mbalimbali yanayohusu Serikali Mtandao. Pia, nawashukuru washiriki wengine wote kwa kukubali kuacha kazi zao nyingine muhimu ili kujumuika nasi kwenye Kikao Kazi hiki.

***Ndugu Mwenyekiti,*** kwa namna ya pekee kabisa ningependa kuwashukuru wenyeji wetu Chuo Cha Sayansi ya Kompyuta, Habari na Mawasiliano, Chuo Kikuu Cha Dodoma kwa kushirikiana nasi kwa hali na mali katika maandalizi ya Kikao hiki.

Aidha, nawashukuru wadau mbalimbali ambao wamefanikisha Kikao Kazi hiki. Kipekee ninaomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Tume ya Sayansi na Technolojia (COSTECH), Benki ya NMB, Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA), Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF), Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), Shirika la Hifadhi ya Jamii (NSSF) Bohari Kuu ya Madawa (MSD) na Mamlaka ya Usimamizi wa Mifuko ya Hifadhi Jamii (SSRA) ambao wamefadhili Kikao Kazi hiki.

***Ndugu Mwenyekiti,*** ninapenda pia kuwashukuru Washiriki waliowasilisha Mada na Tafiti kutoka Vyuo vyetu vya Elimu za juu. Najua mmeahirisha shughuli zenu za masomo, lakini mliona ni vyema mkaja kushirikiana nasi katika Kikao hiki kuonyesha kile mnachoamini kitaweza kusaidia Taifa.

***Ndugu Mwenyekiti,*** ni matumaini yetu kwamba wadau wote wa TEHAMA tutaendelea kuongeza juhudi katika kufanya utafiti na ubunifu na kubadilishana taarifa ili kupata ufumbuzi wa kero tulizoziainisha kwa lengo la kuhakikisha tunapata tija na ufanisi na kuchangia katika ujenzi wa Tanzania ya Viwanda.

***Ndugu Mwenyekiti,*** na washiriki wote naomba tena niwashukuru kwa kushiriki katika Kikao hiki na hususani siku hii; niwatakie jioni njema, na safari njema wakati mkirudi sehemu zenu za kazi.

***Asanteni Sana***